

Obadia

¹ Maono ya Obadia.

Hili ndilo asemalo BWANA Mwenyezi kuhusu Edomu:

Tumesikia ujumbe kutoka kwa BWANA:

Mjumbe alitumwa kwa mataifa kusema,
“Inukeni, twendeni tukapigane vita dhidi yake.”

² “Angalieni, nitawafanya wadogo mionganini
mwa mataifa,
mtadharauliwa kabisa.

³ Kiburi cha moyo wako kimekudanganya,
wewe unayeishi katika majabali ya miamba
na kufanya makao yako juu,
wewe unayejiambia mwenyewe,
‘Ni nani awezaye kunishusha chini?’

⁴ Ingawa unapaa juu kama tai
na kufanya kiota chako kati ya nyota,
nitakushusha chini kutoka huko,”
asema BWANA.

⁵ “Ikiwa wevi wangekuja kwako,
ikiwa wanyang’anyi wangekujia usiku:
Lo! Tazama ni maafa kiasi gani yanakuwa
yanakungojea:
je, si wangeiba tu kiasi ambacho wangehitaji?

Kama wachuma zabibu wangekuja kwako,
je, wasingebakiza zabibu chache?

⁶ Lakini tazama jinsi Esau atakavyotekwa,

jinsi hazina zake zilizofichwa zitatekwa nyara!

- ⁷ Wote ulioungana nao watakuFukuza hadi mpakani,
 rafiki zako watakudanganya na kukushinda,
 wale wanaokula mkate wako watakutegea mtego,
 lakini hutaweza kuugundua.
- ⁸ “Katika siku hiyo,” asema BWANA,
 “je, sitaangamiza watu wenye hekima wa Edomu,
 watu wenye ufahamu katika milima ya Esau?
- ⁹ Ee Temani, mashujaa wako watatiwa hofu,
 kila mmoja katika milima ya Esau
 ataangushwa chini kwa kuchinjwa.
- ¹⁰ Kwa sababu ya jeuri uliyofanya dhidi ya ndugu yako Yakobo,
 aibu itakufunika;
 utaangamizwa milele.
- ¹¹ Siku ile ulisimama mbali ukiangalia wakati wageni walipojichukulia utajiri wake na watu wa nchi nyingine walipoingia malango yake wakipiga kura kwa ajili ya Yerusalem, ulikuwa kama mmoja wao.
- ¹² Usingemdharau ndugu yako katika siku ya msiba wake, wala kufurahia juu ya watu wa Yuda katika siku ya maangamizi yao, wala kujigamba sana katika siku ya taabu yao.

13 Usingeingia katika malango ya watu wangu
 katika siku ya maafa yao,
 wala kuwadharau katika janga lao
 katika siku ya maafa yao,
 wala kunyang'anya mali zao
 katika siku ya maafa yao.

14 Usingengoja kwenye njia panda
 na kuwaua wakimbizi wao,
 wala kuwatoa watu wake waliosalia
 katika siku ya shida yao.

15 "Siku ya BWANA iko karibu
 kwa mataifa yote.

Kama ulivyofanya, nawe utafanyiwa vivyo
 hivyo,
 matendo yako yatakurudia juu ya kichwa
 chako.

16 Kama vile ulivyokunywa juu ya mlima wangu
 mtakatifu,
 vivyo hivyo mataifa yote watakunywa mful-
 ulizo,
 watakunywa na kunywa,
 nao watatoweka kana kwamba hawajawahi
 kuwepo.

17 Lakini katika Mlima Sayuni kutakuwepo
 na wale watakaoookoka;
 nao utakuwa mtakatifu,
 nayo nyumba ya Yakobo
 itamiliiki urithi wake.

18 Nyumba ya Yakobo itakuwa moto,
 na nyumba ya Yosefu itakuwa mwali wa
 moto;
 nayo nyumba ya Esau itakuwa bua kavu,
 nao wataiwasha moto na kuiteketeza.

Hakutakuwa na watakaosalimika
kutoka nyumba ya Esau.”
BWANA amesema.

- 19 Watu kutoka nchi ya Negebu
wataikalia milima ya Esau,
na watu kutoka miteremko ya vilima
watamiliki nchi ya Wafilsti.
Watayakalia mashamba ya Efraimu na Samaria,
naye Benyamini atamiliki Gileadi.
- 20 Kundi la Waisraeli walioko uhamishoni
Kanaani
watarudi na kumiliki nchi mpaka Sarepta.
Walioko uhamishoni Sefaradi kutoka
Yerusalem
watamiliki miji ya Negebu.
- 21 Waokoaji watakwea juu ya Mlima Sayuni
kutawala milima ya Esau.
Nao ufalme utakuwa wa BWANA.

**Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia
Takatifu™ (Bible)**

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 18 Apr 2025 from source files dated 31 Aug 2023

9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462